

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA NANE



11 APRILI, 2019

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA NANE – TAREHE 11 APRILI, 2019

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

62. MHESHIMIWA RICHARD PHILIP MBOGO
(NSIMBO):

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mabadiliko ya Sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa sura 290 yameleta nafuu sana kwa wakulima, lakini wakati huo huo Halmashauri za Wilaya zenye wakulima wadogo zimeathirika kimapato na kusababisha kushindwa kutatua kero za Wananchi kwa wakati:-

(a) Je, Serikali inaweza kuangalia upya suala la utoaji Ruzuku za maendeleo;

(b) Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo imeathirika kwa kiwango kikubwa; Je, Serikali ipo tayari

kuipatia ruzuku ili kutoa huduma za Elimu na Afya.

WIZARA YA MAJI:

63. MHESHIMIWA BALOZI DKT. DIODORUS BUBERWA KAMALA (NKENGE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Mto Kagera ni chanzo muhimu kinachoweza kusaidia upatikanaji wa maji safi na salama kwa Wakazi wanaopakana nao:-

Je, kwa nini Serikali isifanye utaratibu wa kuvuta maji hayo ili yawasaidie Wakazi wa maeneo hayo.

64. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (TARIME MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali imeshindwa kukamilisha mradi wa visima 23 ambavyo vingesaidia kama suluhisho la muda mfupi la tatizo la maji safi na salama katika Mji wa Tarime hususan kwenye maeneo ya Kata za pembezoni kama Nyandoto (Masurula), Nkende, Ketare, Kenyamanyori, Nyamisangura na Turwa;

(b) Mhe. Rais alipofanya ziara Jimbo la Tarime Mjini Julai, 2018 aliwaeleza Wananchi kuwa Serikali imetenga takriban bilioni 14 kwa ajili ya maji kutoka Ziwa Victoria ambayo itaondoa kabisa tatizo la maji katika Mji wa Tarime; Je, ni hatua gani imefikiwa kwenye ahadi hiyo, hasa ikizingatiwa kuwa mradi huo upo kwenye mchakato kwa miaka mingi sasa.

WIZARA YA NISHATI:

65. MHESHIMIWA SILYVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-
Mradi wa umeme mkubwa wa msongo wa KVA 400 toka Kinyerezi kupitia Pwani, Morogoro, Singida na Arusha umechukua maeneo ya Wananchi kwa muda mrefu bila kuwalipa fidia:-

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kulipa fidia hiyo.

**66. MHESHIMIWA SHAMSIA AZIZI MTAMBA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Gesi ambayo imegunduliwa katika Mkoa wa Mtwara itanufaisha Wananchi wote nchini na Taifa kwa ujumla:-

Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kujenga Chuo kitakachotoa mafunzo ya Gesi na Mafuta katika Kanda ya Kusini ili Vijana wa Lindi na Mtwara na maeneo mengine waweze kupata taaluma na kuweza kushiriki kwenye Sekta hiyo.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

**67. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON
MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Maeneo mengi katika Jimbo la Tabora Mjini na Iramba Mashariki hayana mawasiliano ya simu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga minara ya simu katika maeneo hayo ili Wananchi wa maeneo hayo wapate mawasiliano.

III. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI) NA
WAZIRI WA NCHI, OFISI YA (RAIS UTUMISHI NA
UTAWALA BORA):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
11 APRILI, 2019**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**

